



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba kuajiriwa katika nafasi za kazi zifuatazo kujaza ofisi za Wilaya:

### 1.0 AFISA UCHUNGUZI (NAFASI 250)

#### 1.1 Sifa za Mwombaji:

#### 1.2 Sifa za Kitaaluma:

- Muombaji awe angalau na elimu ya shahada ya kwanza iliyotolewa na chuo kinachotambulika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika fani zozote kati ya hizi: **Sheria, Uhasibu, Kodi, Sayansi ya Kompyuta, Sayansi ya Uhalisia, Ununuzi, Uchumi, Mipango, Usalama wa Mitandao, Takwimu, Ukadiriaji wa Majenzi, Uhandisi wa Umeme, Usanifu wa Majengo, Uhandisi wa Ujenzi, Uhandisi wa barabara na Uhandisi wa Maji, Saikolojia, Ushauri na Unasihi;**
- Muombaji awe na ufaulu wa kuanzia daraja la pili la chini (*lower second class*).
- Waombaji waliosajiliwa na Bodi za Kitaaluma watapewa kipaumbele zaidi.

#### 1.3 Sifa zingine:

- Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 30.

## **2.0 MCHUNGUZI MSAIDIZI (NAFASI 100)**

### **2.1 Sifa za Mwombaji:**

### **2.2 Sifa za Kitaaluma:**

- Awe na cheti cha elimu ya Kidato cha nne (CSE) au Kidato cha sita (ACSE), Astashahada au Stashahada ya fani yoyote inayotolewa na Taasisi au chuo kinachotambulika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na fani kama vile Mafunzo ya JKT na stadi za ulinzi, Ufundi wa magari, uhomeleaji na upigaji rangi za magari, Umeme wa magari, Udereva, Usaidizi wa ofisi na Mapokezi, uhasibu wasaidizi, Katibu Muhtasi/Mwandishi Mwendesha ofisi.

### **2.3 Sifa zingine:**

- Mwombaji ni lazima awe raia Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 25.

## **3.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

1. Waombaji wanapaswa kuwa waadilifu na wasiokuwa na rekodi ya uhalifu;
2. Waombaji waambatishe nakala zilizothibitishwa za vyeti vya kitaaluma na nyaraka nyingine ikiwamo nakala za vyeti vya kumaliza masomo katika ngazi mbali mbali za masomo;
3. Waombaji wawe wamepitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa.
4. Waombaji wawasilishe nakala zilizothibitishwa za vyeti husika vikiwamo vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya elimu, vitambulisho vya Taifa (NIDA) au namba ya usajili wa vitambulisho vya Taifa, picha ndogo moja n.k;
5. Shuhuda za walimu, wahadhiri au waajiri kuhusu uwezo wa muombaji kimasomo au kiujuzi ama uzoefu na ufanisi wake katika kazi, nakala za vyeti vya taaluma zisizokuwa kamilifu na slipu za matokeo ya mitihani hazitapokelewa;
6. Vyeti vilivyotolewa na Bodi za Mitihani za nje ya Tanzania vya elimu ya Kidato cha nne (CSE) au elimu ya Kidato cha sita (ACSE) vinapaswa kuthibitishwa na Baraza la Mitihani ya Taifa la Tanzania (NECTA);
7. Vyeti vilivyotolewa na Vyuo Vikuu vya nje ya Tanzania vilivyothibitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) vitapokelewa;
8. Waombaji wanapaswa kuambatisa Maelezo Binafsi (CV) kuhusu elimu, ujuzi na uzoefu wa kazi ya hivi karibuni na yenye anuani ya makazi, anuani

- ya posta, baruapepe na namba za simu za mkononi zinazofikika kwa mawasiliano;
9. Hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya waombaji watakaowasilisha vyeti vya taaluma vya kughushi na taarifa za uongo katika Maelezo Binafsi (CV);
  10. Waombaji wanatakiwa kuwasilisha majina matatu ya wadhamini na namba za mawasiliano zinazopatikana na nakala moja ya picha ya hivi karibuni ya kila mdhamini;
  11. Waombaji waliowahi kuajiriwa katika Utumishi wa Umma na kuachishwa kazi kwa sababu zozote zile wasiwasilishe maombi;
  12. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono katika lugha ya Kiswahili au ya Kiingereza;
  13. Waombaji ambao ni waajiriwa katika Taasisi za Serikali wapitishie maombi kwa waajiri wao wa sasa.
  14. Waombaji watakaokidhi vigezo vya awali vya sifa na matakwa ya maombi ndiyo pekee watakaofuzu kuingia katika hatua nyingine za mchakato huu wa ajira.

#### **ANGALIZO:**

1. **Waombaji wote watambue kuwa ikitokea wameajiriwa watapangwa kwenye kituo chochote cha kazi kadri ya uamuzi wa Mkurugenzi Mkuu.**
2. **Cheti cha uanachama wa Klabu ya Wapinga Rushwa kitakuwa na faida ya ziada.**

#### **4.0 JINSI YA KUWASILISHA MAOMBI**

- Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielekitroniki wa ajira wa TAKUKURU ambao anuani yake ni: [www.pccb.go.tz/ajira](http://www.pccb.go.tz/ajira) na si vinginevyo. **Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kwa mkono hayatapokelewa.**
- Barua za maombi ya ajira ziandikwe kwa Anuanwi;  
**Mkurugenzi Mkuu,**  
**Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa,**  
**Mtaa wa Jamhuri,**  
**S.L.P. 1291,**  
**41101 DODOMA.**

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI: Tarehe 20 Februari, 2024**